

Maboresho ya kanuni kubana madereva

Na Mwandishi Wetu

RASIMU ya Kanuni za Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) za Usimamizi wa Madhara ya Uchovu kwa Madereva za mwaka 2025 zinabana madereva wa safari ndefu ikiwa ni pamoja kuwazuia kuendesha chombo cha abiria kwa zaidi ya saa tisa ndani ya saa 24.

Pia, kanuni hizo zinazuia dereva kuendesha chombo kwa zaidi ya saa tano mfululizo bila kupumzika.

"Dereva hataruhusiwa kuendesha chombo kwa zaidi ya saa 48 ndani ya siku saba mfululizo," imeeleza rasimu hiyo.

Tangu Machi 17, mwaka huu Latra inapokea maoni ya kuboresha kanuni hizo na kazi hiyo inafanyika kwa wiki mbili.

Kanuni zinamtaka dereva achukue mapumziko ya lazima angalau saa 10 ndani ya saa 24.

Pia, dereva wa gari la abiria anatakiwa apumzike dakika 30 baada ya kuendesha kwa saa tano mfululizo na pia apumzike kwa saa 24 mfululizo ndani ya siku saba za kazi.

Kanuni zinamtaka mtoa huduma atahakikishe dereva mwenza wa mabasi yaendayo masafa marefu atakuwepo kwenye kituo cha kubadilishana kwa ajili ya kupokea basi kutoka kwa dereva aliyeendesha kwa saa nane mfululizo kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Usimamizi Madhara ya Uchovu.

"Mtoa huduma atahakikisha kwamba dereva wa chombo vya kukodi, na magari ya mizigo na mabasi ya mijini anapata muda wa kupumzika au kubadilishana na dereva

mwingine baada ya saa nane za kuendesha gari kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Kudhibiti Madhara ya Uchovu," zimeeleza kanuni.

Adhabu

Kanuni zinaeleza mwenye leseni atakayekiuka mojawapo ya masharti ya kanuni hizo atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia atalipa faini isiyopungua Sh 200,000 lakini isiyozidi Sh 500,000 au kifungo kisichopungua mwaka lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

"Dereva atakayekiuka mojawapo ya masharti ya kanuni hizi atakuwa ametenda kosa na akikutwa na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi laki moja lakini isiyozidi Shilingi laki mbili za Tanzania, au kifungo kisichopungua mwaka mmoja lakini kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja," zimeeleza.

Machi 17, mwaka huu Mkurugenzi Msaidizi Usafiri kwa Njia ya Barabara, Wizara ya Uchukuzi, Andrew Magombana alisema maoni ya wadau ni nyenzo muhimu kuboresha kanuni hizo.

Magombana alisema kanuni hizo zinalenga kuhakikisha madereva wa vyombo vya moto kibiashara wanaendesha wakiwa na utimamu wa mwili na akili ili kupunguza ajali za barabarani.

"Kanuni hizi zinalenga kuhakikisha madereva wanafanya kazi wakiwa na afya bora ya mwili na akili. Tukifanikiwa kudhibiti uendeshaji katika hali ya uchovu, tutakuwa tume-punguza kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani pamoja na usumbufu kwa abiria," alisema.